

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**Verbatim Report Of**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL**

**ELDAMA RAVINE CONSTITUENCY AT ELDAMA RAVINE TOWN  
HALL**

**ON**

**17<sup>TH</sup> OCTOBER 2002.**

*Transcribed by Chepkemai Catherine.*

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, RIFT VALLEY PROVINCE, ELDAMA RAVINE  
CONSTITUENCY AT ELDAMA RAVINE TOWN HALL ON 17<sup>th</sup> OCTOBER 2002**

**Present:**

Wycliffe Owade - P.O acting on behalf of Commissioner Dr. Andronico Adede.

**Secretariat Staff in attendance:**

1. Esther Mugo            Assistant Programme Officer
2. Alice Thuo            Verbatim Recorder
3. Paul Tuikong          District Coordinator

The meeting started at 11:45 a.m.

**Paul Tuikong:** Basi ninafikiri kwa wakati huu tungeanza mkutano wetu, ninaona saa imeenda. Tutaita mtu mmoja atuongoze kwa maombi ili tupate kuendelea. Sally, tafadhali uje utuombe.

**Sally: (Prayer)** Tuombe. *Mungu Baba Katika jina la Yesu Kristo, tunashukuru asubuhi ya leo, asante Mungu wetu kwa sababu umetuongoza na umetulinda. Asante kwa sababu umetutoa kwa manyumba zetu mpaka tumefika mahali hapa tukiwa wazima. Kwa hivyo tunakushukuru na tunasema ni asante Mungu wetu. Asante hata kwa ajili ya Asubuhi ya leo, ya kwamba Mungu tumekusanyika mahali hapa kwa lengo moja ya kwamba tunaenda kuketi na*

*kujadiliana kuhusu Katiba ya nchi yetu. Kwa hivyo Mungu wetu tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu apate kutuongoza. Tunapojadiliana Baba tunaomba utupe hekima na maarifa katika maisha yetu, ya kwamba tunaenda kusema mambo ambayo yatatuelekeza karibu na wewe Mungu wetu na hata yale yote ambayo tutaenda kuongea juu yake, utupe hekima na maarifa katika maisha yetu ya kwamba tunaenda kusema mambo ambayo yatatuelekeza karibu na wewe Mungu wetu. Hata yale yote ambayo tutaenda kuongea juu yake, Baba tunaomba ya kwamba wewe ndiwe utakae tuongoza na hata kutupa ufahamu na mwelekeo katika nchi yetu. Asante Mungu wetu kwa sababu ya kila mmoja ambaye ameketi mahali hapa siku ya leo. Tunajua kwamba kila mtu ako na jambo la kusema na kwa hivyo tunaomba ya kwamba upate kutupa hekima na maarifa katika mambo haya yote ili tunaposema, tuiseme mambo ambayo Bwana yatatuelekeza mahali ambapo hapatakuwa pa mafanikio katika nchi yetu. Asante kwa sababu Mfalme wetu unajali na hata unatupenda. Ninaomba yote nikiamini katika jina la Yesu aliye Mungu wetu na aliye mwombezi wetu.*

**Audience:** Amen.

**Paul Tuikong:** Wageni wetu kutoka Nairobi, CKRC, wakiongozwa na Bwana Wycliffe Owade ambaye ni Programme Officer katika ofisi kuu kule Nairobi pamoja na wale ambao wameandama pamoja, Committee members wangu, ambao wako hapa, delegates ambao watawakilisha Koibatek kule Nairobi during the National Constitutional Conference, Civic education providers ambao wako hapa, viongozi wa serikali, Councillors, viongozi wa tabaka mbali mbali, wananchi wote wa eneo la Uwakilishi Bungeni la Eldama Ravine, Hamjambo?

**Audience:** (Response by clapping)

**Paul Tuikong:** Ninataka kuchukua nafasi hii kuwakaribisha nyinyi hapa siku ya leo, ninajua ni siku ambayo tumekuwa tuingoja sana, ni siku ya muhimu sana katika area hii yetu ya Koibatek na ninataka kuwashukuru kabisa kwa sababu mmekuja mapema ili muje tujadiliane kuhusu Katiba mpya. Na kabla ya hiyo, nitachukua nafasi ya dakika mbili, tatu, kuwajulisha wale ambao tumekuwa tukifanya kazi pamoja tangu tulipoanza kazi ya Katiba katika nchi hii yetu.

Kwanza niko na Committee members, wale wako hapa wasimame niwajulishe kwa officers wetu kutoka Nairobi na wakaaji wa eneo hili la Uwakilishi Bungeni la Eldama Ravine. Tafadhali msimame, committee members wale wako hapa, very good. Councillor David Morogo is the Chairman of the 3Cs Eldama Ravine Constituency, thank you very much. Mama Lydia Bett, yeye ni committee member akiwakilisha eneo hili la Eldama Ravine, Bwana George Githua, pia ni committee member wangu, ambaye tulikuwa tukifanya kazi pamoja. Tuko na wale ambao wamekuwa walimu wa Katiba na wako wengi hapa na ningeliza msimame pahali popote mnapokaa, ndiyo watu wajue mmekuwa mkifanya kazi mzuri. Bwana Timothy Sanga, asante sana, kutoka Boror Youth, Bwana Kiprop, Sanga anafanya na huyo, ni group moja na huyu John Kipkesbai, asante. Huyu ni Bwana Kiprop, group yake imekuwa ile wanajiita Kiplombe village. Nimekuwa na wengine pia kutoka Mogotio, Bwana Kiptum

amekuwa akifanya, weka mkono wako Kiptum, civic education across the district; both Mogotio and Eldama Ravine.

Ninafikiri kwa wakati huu, vile nyinyi mnajua juzi tulifanya kazi ingine na mlikuwa mkisoma kwa magazeti ya kwamba watu watatu walikuwa wanatakikana kuwakilisha Koibatek District kule Nairobi during the NCC na tulifanya kazi hiyo ya uchaguzi na tayari tuko na wale ambao watatuakilisha kule Nairobi. Ningeomba wasimame halafu niwa-introduce. Bwana David Kimaiwa Kigen, Councillor kutoka upande wa Koitebes, delegate wa kwenda Nairobi. Huyu ambaye mnamuona anaitwa Pastor Resally Chepkoech, yeye ni delegate na anatoka upande wa Mumberes na anaelekea Nairobi for the NCC. Kuna mwingine ambaye ataungana na sisi, huyo ni Bwana Kiptingos, pia ni mmoja wa wale watatu ambao wataenda Nairobi. Hawa wote ni watu ...wale wako hapa mbele yako Bwana Owade, ni watu ambao tumekuwa tukifanya kazi pamoja tangu wakati ule.

Tunajua ya kwamba barabara imekuwa mdefu; tulianza na establishing the office, tukaanza na constituency forums, tulifanya forums mingi sana across the district, tulienda mpaka almost village to village level na basi ukiwaona hawa ni stakeholders ambao tumekuwa all through civic education. Kuna hata wale - simama Mr. Mwaura - Mr. Mwaura pia ni civic education supervisor lakini not from CKRC but from ICEP, they have been doing a good job also. So ni hawa tumekuwa tukisaidiana on civic education, tukakuja public hearings, hawa ndio watu ambao tulikuwa na hao hapa na ninakumbuka kabisa ilikuwa tarehe tano mwezi wa saba, tulikuwa hapa tukipeana maoni juu ya Katiba Mpya.

Maoni yenu, yale mlipiana tarehe tano mwezi wa saba, Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya walienda waka-record maneno yenu yote, tuko na report ya Eldama Ravine Constituency. Yale ambayo mlisema hapa, tarehe tano, yako hapa yote na ofisi yangu tume photocopy moja ya hii tukaweka kwa ---(Inaudible) na ingine tukaweka Koilegen. So kuna copy moja Koilegen na kuna copy moja kwa ---(Inaudible) Ukitaka Report ya Eldama Ravine, unaweza kwenda ku-photocopy kule, uone vile watu wa Eldama Ravine walisema. Iko profile hapa ya district, mtajisomea, population na hayo yote, hata vile uchaguzi ulivyoendelea 1997, iko hapa, nani alipata nini, iko hapa yote, hata vile tulipeana maoni yetu. Wale watu ambao walipeana maoni hapa walikuwa watu mia moja, wanaume wakiwa themanini na nane halafu wamama tisa halafu wengine watatu hawakuweka ni nani halafu kuna individual institution na hayo yote. This report is very good for you, ukiwa na nafasi unaweza kwenda Koilegen ama kwa ---(Inaudible) ukipatie copy moja .

Basi tumefika kiwango kingine kwa sababu tulipokuwa hapa wakati mwingine, mwezi wa saba, tuliwaambia ya kwamba Commissioners wanakuja kuchukua maoni yetu halafu waende waandike Draft report. So the draft report tayari imetokea, mko nayo hapo, everybody who is here ningeomba uwe na copy yako, hiyo itakuwa yako mwenyewe, na utaenda nayo, baada ya hapa utaenda nayo, huwezi kurudisha, hiyo ni yako.

Mwezi wa nane Commissioner walikuwa Mombasa wakiandika hiyo na tayari imetoka. This is not the final draft, si ya kwamba hii imekuwa Katiba, hapana. Bado iko katika Draft, kurekebisha bado iko nafasi, tunarekebisha kuanzia sasa,

itarekebishwa kwa NCC so tusije tukasema ya kwamba... notion ambayo imekuwa na watu wengine ni kwamba Katiba tayari imeandikwa. Haijaandikwa kwa sababu tuko hapa leo kwa minajili ya kuangalia na kuona ni sehemu gani imekuwa sawa, ninyi ndio mtasema na wale ambao wako hapa wataendelea nayo kule Nairobi, kuchukua na kupeana.

Ili nisimamishe mgeni wetu siku ya leo, ningetaka ku-introduce yeye namna hii, ya kwamba kazi hii ambayo tunafanya siku ya leo ni kazi ambayo inaendelea kote nchini Kenya. Ilianza wiki iliyopita, Jumatatu, ilianza last week on Monday na every constituency inatembelewa. Jana tulikuwa Mogotio, tumemaliza na Mogotio na leo ni Eldama Ravine. Kote nchini Kenya, hata Baringo, jana nilisikia coordinator wa Baringo alikuwa Kabartonjo na leo ninafikiri wako Baringo East. So, hii kazi inaendelea kote nchini Kenya, si ya kwamba ni hapa Koibatek peke yake. Infact, tunapooonga, we are about the last, tunamaliza. By Friday hii kazi itakuwa imemalizika kwa sababu according to our programme, wiki ijayo itakuwa preparations ya the National Constitution Conference ambayo tunatarajia ya kwamba 28<sup>th</sup> ndiyo itakuwa siku ambayo the first, from 28<sup>th</sup> na inaendelea mbele pengine one month, ndiyo conference itaanza.

So, tukiwa hapa leo, ni kazi ambayo inafanyika kote nchini Kenya, mjue hiyo. Constituencies ni mingi so Commissioners wengine wameenda Constituencies zingine, programme officers ni deputies wa Commissioners so pia wako na information ya kutosha ile mngelitaji ichukuliwe watafanya hivyo. Tungekuwa na Commissioner Andronico Adede, the new Commissioner, angekuja hapa leo lakini nilipopiga simu nikaambiwa ya kwamba alikuwa anatakikana aende Geneva, nafikiri he is even in Geneva by now, Geneva I don't know ni Switzerland au wapi, but as we are talking now he is in Switzerland, so wakatuma Mr. Wycliffe Owade ambaye ni Programme officer wetu katika Nairobi aje amwakilisha and I am very sure he is very able. Tulikuwa naye jana, he is very able na hata nyinyi baada ya hii kazi mtasema he has done a good job.

I don't want to take a long time, wale wako pale, watasema majina yao halafu tumpatie Mr. Owade aendele. Just say your name.

**Esther Mugo:** I am Esther Mugo

**Paul Tuikong:** What you are doing?

**Esther Mugo:** ----(not clear) kazi yangu ni ku-record everything that is happening here. I am the Assistant Programme Officer.

**Alice Thuo:** Kwa majina ni Alice Thuo. Kazi yangu ni ku-record yale maneno mnasema kwa tape recorder.

**Paul Tuikong:** Munaona hii kitu hii, inazunguka so this thing inazunguka namna hii, it will be replayed, kusikiza watu wa Eldama Ravine walisema nini. So this one will be replayed in Nairobi so chochote ambacho tutasema, mjue ya kwamba

imekuwa recorded, it has been recorded.

May I welcome Mr. Owade to introduce himself also na aendelee from hapo.

**Wycliffe Owade:** Hamjambo wananchi wa Eldama Ravine?

**Audience:** *(Response through hand clapping)*

**Mr. Owade:** Kwa jina kama mlivyosikia ninaitwa Wycliffe Owade. Ningeanza kwa kusema ninaomba mnipee ruhusa niketi chini ili ndiyo tujadiliane vizuri, hata ingawa mimi bado kijana lakini saa zingine hii kitu si rahisi. Nimepatiwa ruhusa?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Asante sana. Sasa nataka tuangalie hiyo pull out yetu, nitasema kwa Kiswahili na Kizungu pia ili twende haraka haraka. Hiyo ni sawa? Sasa ukiangalia hiyo, mwanzo mwanzo hapo, tuko na yaliyomo, that is utangulizi na inaenda mpaka chapter 20. Kwa hivyo ningeomba tutulie kabisa na tusikie kwa makini na ukiwa na maoni, hii ni mswada tu vile coordinator amesema. Sasa sisi kazi yetu hapa ni kusoma halafu nyinyi mnasikia na mkiwa na maoni tofauti mtapatiwa hiyo time ambayo mtasema hii tunaona ingekuwa hivi ama hii tumekataa kabisa. Mko na ule uhuru na demokrasia ya kusema kwa sababu hii ni mswada, si ile Katiba. Tuko pamoja?

**Response:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Basi tuanze hapo page two, page two imeandikwa hapo table of contents, hapo chini tuko na Preamble, yaani utangulizi maana yake hii ndilo jiwe la msingi wa Katiba wa Kenya. Ndiyo Wakenya wengine walitoa maoni kwamba lazima tuwe na utangulizi kwa Katiba yetu na nitasoma kwa Kiswahili. Na inasema hivi;

“Sisi wananchi wa Kenya tukifahamu wingi wa tofauti zetu za kikabila, kitamaduni na kidini, na tukidhamiria kuisha kwa amani kama taifa moja huru lisilogawika, pili, tukijitolea kulenda na kulinda maslahi ya kila moja, familia na jamii katika taifa letu, tukitambua matumaini ya wanawake na wanaume wetu ya kuwa na serikali ambayo imejengwa katika msingi muhimu inayodhamini uhuru, demokrasia, haki ya kijamii na utawala wa kisheria tukitekeleza haki yetu isiyotengeka ya uhuru ili kuamua aina ya utawala wa nchi yetu na ikiwa tumeshiriki kikamilifu katika utaratibu wa kuandaa Katiba. Tunaikubali, tunaifanya sheria na tunaitoa kwetu wenyewe na kwa vizazi vyetu vijavyo Katiba hii. Mungu ibariki Kenya”

Sasa hiyo ndiyo utangulizi, yaani jiwe la msingi la hii Katiba yetu. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Halafu, I want us now to go to page 4, tuko na chapter 1, sovereignty of the people and supremacy of the Constitution yaani kwa Kiswahili, uhuru wa wananchi na ukuu wa Katiba. Inasema hivi, nitasoma kwa Kiswahili; Uhuru wa wananchi, Katiba mpya inasema hivi: Article 1:1. “Mamlaka yote ya uhuru ni ya wananchi wa Kenya na yanaweza kutekelezwa tu kulingana na Katiba” 2. “Wananchi watatekeleza uwezo wao wa uhuru kwa njia ya moja kwa moja au kupitia kwa wawakilishi wao watakao teuliwa kidemokrasia” 3. “Mamlaka ya uhuru ya wananchi yamegawanywa kwa njia tofauti miongoni mwao

- (a) Bunge, ambamo wananchi wameweka amana ya mamlaka ya kisheria ya jamhuri ili yatekelezwe kwa mujibu wa sura ya saba.
- (b) Mamlaka ya nchi ambamo wananchi wameweka amana ya mamlaka ya jamhuri ili yatekelezwe kwa mujibu wa sura ya nane.
- (c) Mahakama na mahakama nyingine huria zizizopendelea ambazo kwazo wananchi wametoa amana ya mamlaka ya kimahakama ili yatekelezwe kwa mujibu wa sura ya tisa.
- (d) Tume za kiKatiba na ofisi ambazo zimeundwa na sura ya kumi na saba na kwingine katika Katiba ambazo kwazo wananchi wametoa amana ya kulinda na kujenga jamhuri ya kiKatiba ambayo inaweza kupatikana kutokana na utekelezaji wa vyombo vyenye majukumu na uwezo vilivyowekwa na Katiba.

Sasa hiyo ndiyo maana ya uhuru wa wananchi. Nyinyi wananchi ndio mmepatia hiyo Katiba mamlaka. Hiyo ni kweli ama uwongo?

**Audience:** Ni kweli.

**Mr. Owade:** Mamlaka yote ya uhuru wa nchi hii inatoka kwa wananchi wa Kenya na sasa hiyo sura ya kwanza ama chapter one inaongea juu ya uhuru wa wananchi na ukuu wa Katiba. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Ya pili ama chapter two, Jamhuri; tunataka kujua Katiba Mpya inasema nini kuhusu the republic. Republic maana yake ni nini? Hebu tuangalie hapo na tusome article 6:1 Jamhuri ni nini? “Kenya ni jamhuri iliyo huru.

2. Jamhuri ya Kenya imejengwa katika msingi wa kijamhuri wa utawala mwema kupitia demokrasia ya vyama vingi, utawala shirikishi, uwazi na uwajibikaji, utekelezaji wa madaraka, heshima kwa haki za binadamu, uhuru wa kimsingi na utawala wa sheria.” Hiyo ndiyo maana ya republic, yaani jamhuri. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Ndiyo. Halafu twende kwa article 9:1, eneo na makao makuu, hiyo mnaweza kusoma. Twende kwa article 9:1; Languages yaani lugha. Katiba mpya inasema nini kuhusu lugha? Article 9:1, hiyo ni page 4; “Lugha rasmi za Kenya ni Kiswahili na Kiingereza na nyaraka zote rasmi zitatolewa katika lugha hizi mbili. 2. Lugha ya taifa ya Kenya ni Kiswahili 3. Serikali itaheshimu na kulinda wingi na tofauti za lugha za wananchi wa Kenya na itakuza maendeleo na matumizi ya Kiswahili, lugha za asili, lugha ishara na Braille. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Haya! Twende kwa taifa na dini, article 10:1, that is the same page 4; “taifa na dini vitatenganishwa. 2. hapatakuwa na dini ya taifa 3. serikali itazichukulia dini zote kwa usawa.

Alama za taifa, article 11: ‘ alama za taifa za jamhuri ya Kenya ikiwemo; 1. Pendera ya taifa. 2. wimbo wa taifa. 3. Nembo na 4. muhuri wa taifa la Kenya, ni kama ambavyo zimeelezwa katika nyongeza ya tatu.

Twende kwa siku za taifa: Article 13:1; kwa Katiba hii mpya, tumependekeza hizo ziwe siku za taifa, hata ingawa tutawa na zile siku tunaita public holidays, hapa tuko na zile tunaita National Holidays na zitakuwa zifuatazo. “Siku zifuatazo zitazingatiwa kama siku kuu za taifa;

- (a) Juni 1; siku kuu ya Madaraka
- (b) Disemba 12; siku kuu ya Jamhuri
- (c) Siku ya Katiba kufanywa kuwa sheria; siku kuu ya Katiba

Hizo zitakuwa national holidays lakini pia tutakuwa na public holidays ambazo hatujaweka hapa.

Baada ya hiyo twende kwa chapter 3, national goals, values and principles: Malengo ya taifa, maadili na kanuni; kila taifa lazima liwe na malengo yake na inasema huvi, article 14:1 “malengo ya taifa, maadili na kanuni zilizomo katika sura hii zinahusu mamlaka ya Nchi, Bunge, Mahakama, Tawala za Wilayani na vyombo vingine vya serikali na viongozi, raia na miungano ya kibinafsi, pale ambapo chombo ni mojawapo ya hizo ambazo zimeandikwa hapo” Mnaweza kusoma.

Sasa hizo ndizo malengo yetu kama taifa moja. Lazima tuwe na malengo, lazima tuwe na maadili na kanuni kuongoza Nchi hii tukufu yetu ya Kenya. Halafu tusome hiyo Chapter 4; Citizenship ili tujue sheria inasema nini kuhusu uraia. Ukiwa na maoni unaweza tu kuandika ama kuweka, saa ile tutawapa nafasi, mtatoa. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Chapter 4 on citizenship, uraia; kanuni za kijumla kuhusu uraia, article 16:1 “isipokuwa pale Katiba imeweka masharti tofauti, raia wote wa Kenya

- (a) wana haki sawa ya kupata haki, fadhila na faida za uraia.
- (b) wana kiwango sawa cha wajibu na majukumu ya uraia
- (c) wana haki sawa ya kupata paspoti ya Kenya na kupata hati yoyote ile ya kitambulisho inayotolewa na serikali kwa uraia.

Tuone sasa hizo categories za kupata uraia, that is article 18: Acquisition of citizenship, tuone inasema nini. Kupata uraia; “uraia unaweza kupatikana kwa njia ya

- (a) kuzaliwa
- (b) kusajilishwa
- (c) kuandikishwa

Halafu tuone inasema nini. Uraia kwa kuzaliwa; article 19:1 “kila mtu aliyezaliwa baada ya utekelezaji wa Katiba atakuwa raia wa Kenya ikiwa wakati wa tarehe ya kuzaliwa mtu huyo, mama ama baba yake ni raia wa Kenya. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Number 2. “mtu aliye raia wa Kenya kuambatana na ibara hii hawezi kupokonywa uraia wake.

Uraia na ndoa: Tuone Katiba mpya inasema nini. Article 20:1; “mtu aliyefunga ndoa na raia wa Kenya kwa kipindi kisicho pungua miaka mitatu ana haki ya kusajilishwa kama raia wa Kenya akituma ombi.

(b) uraia haupotei kwa njia ya ndoa ama wakati wa talaka. Tuko Pamoja?

Uraia kwa kuandikishwa: Article 21 inasema hivi; “mtu aliyekuwa mkaazi wa Kenya kisheria kwa mfululizo na kipindi kisichopungua miaka saba na ambaye anatosheleza masharti yaliyotolewa na sheria ya Bunge, anaweza kutuma ombi la kuwa raia wa Kenya kwa kuandikishwa.

Halafu tuangalie hii Katiba mpya inasema nini kuhusu watoto wanaopatikana Kenya na watoto wa kupanga; article 22:1 “mtoto anayepatikana Kenya, ambaye yuko chini ya umri wa miaka minane ambaye wazazi wake hawajulikani atachukuliwa kuwa raia wa Kenya

(b) Mtoto aliye na chini ya miaka kumi na nane ambaye anaishi na raia wa Kenya ana haki ya kuwa raia wa Kenya anapotuma ombi.

Tuone hapo uraia mara dufu; Dual citizenship: Tulipotembelea pembe zote za Kenya, tulipata maoni kuwa kama wale ndugu

zetu Waturkana, Somali, wale wako kwa mipaka na nchi zingine, kwa border, wao pia walikuwa na maoni yao na Commission ime-recommend hivi kuhusu uraia mara dufu. 23:1 “uraia mara dufu unaruhusiwa chini ya sheria za Kenya.

(b) mtu anayepoteza uraia wa Kenya kwa ajili ya kupata uraia wa nchi nyingine kabla ya kutekelezwa kwa Katiba hii ana haki ya kusajiliwa kama raia wa Kenya anapotuma ombi lake.

(c) mtu anayepoteza uraia wa Kenya kwa ajili ya kupata uraia wa nchi nyingine, anapoacha uraia wa nchi ile ingine atakuwa na haki ya kurudia uraia wake wa Kenya aliofurahia mwanzo.

Kuachishwa uraia; article 24: “mtu atapokonywa uraia wa Kenya ikiwa tu ameupata uraia huo kwa udanganyifu, wasilisho la uwongo, kuficha kwa hoja muhimu ama kwa njia nyingizo kinyume cha sheria. Sasa hiyo ndiyo inahusu kuachishwa uraia. Nyingine unaweza kusoma.

I now want to take you to page 6 on the Bill of Rights, chapter 5 yaani sheria ya haki: Again as we were criss crossing all the Constituencies in this Country, Kenyans really felt that most of them are not aware of their rights. That it is high time these rights are highlighted, it is also high time these rights are protected by the state because if you know your rights, then you know you belong to a democratic state. Is it okay?

**Audience:** Yes.

**Mr.Owade:** Therefore it is important in this century that at this level of political maturity in Kenya, Kenyans should be fully aware of their rights and apart from that these rights must be protected by the state. So having listened to those views, the Constitution of Kenya Review Commission came up with the following recommendations and I would like to read Article 29:1 and 2 just to give you a highlight on what the Bill of Rights is all about na nitasoma kwa Kiswahili.

Article 29:1 Haki za kimzingi na uhuru; “sheria ya haki ndiyo nguzo ya msingi wa serikali ya kidemokrasia na ni muundo wa ukabalifu wa sera za kijamii, kiuchumi na kitamaduni.

(b) madhumuni ya kutambua na kulinda haki za binadamu ni kuhifadhi hadhi ya utu kwa watu binafsi na jamii na kuhitimisha vipawa vya binadamu wote.

Having said all that, I want now to take you to Article 32:1 because article 30 is simply talking of the duty of the state to promote rights, you can see that and you can read it. Let me take you to article 32:1 tuone Katiba Mpya inasema nini. The same page 6. Are we together?

**Audience:** Yes.

**Mr. Owade:** Right to life, yaani haki ya kuishi. Katiba mpya inasema hivi; “Kila mtu anahaki ya kuishi

(b) Hukumu ya kifo imefutuliwa mbali” hiyo ni recommendation ya Katiba hii.

Tuende kwa Article 33: Usawa, equality: Inasema hivi; Kila mtu yuko sawa mbele ya sheria na ana haki sawa ya kulindwa na usawa wa mafikirio ya sheria.

(b) Usawa unajumulisha kufuraia kikamilifu usawa wakati wote na uhuru wote.

Article 34; uhuru kutokana na ubaguzi, yaani freedom from discrimination na inasema hivi: “serikali haitabagua kwa maonevu ya moja kwa moja ama kwa njia isiyokuwa dhahiri dhidi ya mtu yeyote kwa sababu moja au zaidi pamoja na jamii, jinsia, uja uzito ndoa, kabila ama hali ya kitabaka, rangi, umri, ulemavu, dini, dhamira, imani, utamaduni, lugha, ama kuzaliwa. Hiyo Article inaongea juu ya uhuru kutokana na ubaguzi.

Halafu kuna vikundi vingine kati yetu kama binadamu wananchi wa Kenya ama raia ambao sasa Katiba inatoa recognition na ningependa kusoma Article 35:1, wanawake tunataka kujua Katiba hii mpya inasema nini na tutasoma kwa Kiswahili “wanawake wana haki ya kutendewa sawa na wanaume pamoja na fursa sawa katika siasa, uchumi na shughuli za kijamii.

(2) wanawake wana haki ya kupewa hadhi ya utu sawa kama ile inayopewa wanaume.

(3) wanawake na wanaume wana haki sawa za kurithi, kupata nafasi sawa ya kupata na kuthibiti mali.

4. sheria, utamaduni, desturi ama mila zozote zinazozorotesha hadhi, utu, ustawi na maslahi ama hali ya wanawake zinapigwa marufuku.
5. Serikali (a) serikali itawalinda wanawake na haki zao kwa kuzingatia hali zao maalumu na jukumu lao la kuwa mama katika jamii  
(b) itatoa vifaa vinavyotosheleza na fursa ya kuendeleza maslahi ya wanawake ili kuwawezesha kufikia upeo wa vipawa vyao na maendeleo

Halafu kuna watu wengine wazee katika jamii. Katiba mpya pia ime-recognize role ya wazee kwamba lazima walindwe na lazima wapatiwe huduma ile inayotosha kwa sababu wazee wana hekima, wana heshima na lazima tuwape heshima yao. Kwa hivyo tuangalie hapo sheria inasema nini kuhusu wazee katika jamii. Article 36:1.

“wazee katika jamii wana haki ya kuendelea kufurahia haki zote na uhuru kama ilivyo fafanuliwa katika sheria za Kenya pamoja na haki ya;

- (a) kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii
  - (b) kufuatilia maendeleo yao ya kibinafsi
  - (c) kuwa huru kutokana na aina zote za ubaguzi, unyanyasaji au dhuluma
  - (d) kuishi kwa heshima na utu
  - (e) kubaki na uhuru wao.
2. “wanachama wazee katika jamii wana haki ya kuchungwa vyema na kupata usaidizi wa familia na serikali.
  3. “wazee katika jamii wana wajibu wa kufanya mpango kuhusu kustaafu kwao, kugawia watu wengine ujuzi na ustadi wao na

waendeleo kujihusisha na shughuli katika jamii.

4. wizara zinazohusika na vyombo vinavyopokea malalamiko pamoja na Tume ya haki za binadamu na haki za kiutawala --- zitachukua hatua maalum ya kujitayarisha ili kuelewa na kushughulikia mambo yanayowadhira wazee.

Sasa hivyo ndivyo Katiba mpya inasema kuhusu wazee. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Tuone Katiba mpya inasema nini kuhusu watoto na nitasema kwa ufupi. Article 37:1. “Watoto wana nafasi maalum katika jamii. Ni jukumu la wazazi wao, ukoo, jamii na serikali kuwalea, kuwalinda na kuwaelimisha ili waweze kuendelea katika mazingira salama na dhabiti na katika hali ya furaha, upendo, heshima na maelewano na waweze kupimisha upeo wa vipawa vyao katika hali zote; kimwili, kiakili, kihisia na kiroho kwa manufaa yao wenyewe na jamii kwa jumla. Ukisoma hiyo itakuonyesha jinsi Katiba inasema kuhusu maisha ya watoto.

Halafu mkiangalia hapo article 38-ambayo pia inaongea kuhusu familia kwa sababu familia ndiyo msingi wa taifa. Katiba mpya inasema hivi, Article 38:1 “ serikali itambue familia kuwa ndiyo msingi wa umoja wa kijamii na ndiyo msingi muhimu wa taratibu za kijamii.

2. familia inastahili heshima na ulinzi wa serikali

3. kila mtu mwenye angalau umri wa miaka kumi na minane,

(a) ana haki ya kuoau au kuolewa kulingana na makubaliano ya wanaohusika

(b) ana haki ya kuanzisha familia

4. makundi yanayo oana yana haki sawa katika ndoa wakati wa kuoana kwao na katika kuvunja ndoa yao. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Haya! Tuone walemavu, Katiba mpya inasema nini? Article 39:1 “walemavu wana haki ya kufurahia haki zote na uhuru wote uliotajwa katika mswada huu wa sheria na kushiriki kikamilifu katika jamii kama wengine. Tuko pamoja? Na mkisoma hapo mtasikia Katiba mpya inasema nini kuhusu walemavu.

Tuanguzie Article 44, the same page 7: Uhuru wa dini, imani na maoni; inasema hivi “kila mtu ana haki ya uhuru wa dhamira, dini, mawazo, imani na maoni” Sasa hiyo ndiyo inaongea juu ya dini, imani na maoni. Inge mnaweza kusoma baadaye.

Tukianguzie page 8, hapo it is talking about freedom of expression, publication of opinion and access to information na tena inaongea juu ya freedom of association yaani uhuru wa kutoa maoni, uchapishaji wa maoni, kupitia habari na uhuru wa

kushirikiana. This page inaongea juu ya uhuru hizo na unaweza kusoma lakini ningependa kusoma ya kwamba Katiba mpya inasema kila raia wa jamhuri ya Kenya ana haki ya kuona ama kusoma vyombo vyote vya habari. Kama ni KBC, kama ni KTN, kama ni Nation, kama ni nini, mna haki ya kuona, haki ya kusikia, haki ya kusoma halafu nyinyi wenyewe ndio mtakuwa na maoni yenu kwamba decision yenu iko namna hivi, tumependa hii ama la. Tuko pamoja? Kwa hivyo kila raia wa jamhuri ya Kenya ana haki kwa vyombo vya habari, kwa magazeti, ikiwa ni redio haina gani, KBC, Citizen ama nini, mna haki. Ikiwa ni Nation, Taifa, Standard, mna haki. Ikiwa ni channel gani iko TV, hiyo ni yenu kusikia ama kuona ni nini inatendeka. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Sasa hiyo chapter inaongea kuhusu hizo. I now want to take you to the same page 9 and we are still under the Bill of Rights. If you read that, you will realize that the new Constitution in place is just not talking about your rights, is just not talking about what to expect from the state, is not just talking about the structures of the state but it is also talking about your basic needs as a citizen of this Country. Are we together? What is the new Constitution saying? There are special provisions concerning your basic needs as a citizen of this Country and that you have a right to these basic needs. Are we together?

Sasa tukiangalia hapo page 9, inaongea juu ya huduma, tuangalie hapo article 5-6, usalama wa kijamii, afya, elimu, nyumba, chakula, maji, usafi, mazingira. Those are some of the basic needs and the needs which the state has to provide according to the new Constitution proposed. Are we together? Sasa hizo zingine mnaweza kusoma but I want to take you to consumer rights, Article 64:1 and I want to read it in Kiswahili, yaani haki za wateja. Inasema hivi; “wateja wana haki ya

- (a) Kupata bidhaa na huduma zinazofaa
- (b) Kupata habari inayowafaa ili waweze kunufaika kikamilifu kutokana na bidhaa na huduma.
- (c) Kulindwa afya yao, usalama na maslahi yao ya kiuchumi
- (d) Kulipwa fidia kwa makosa yanayosababisha hasara au majeraha

2. Wanaotoa huduma watajitahidi kutafuta ushauri kutoka kwa wateja na vyama vya wateja kuhusiana na maswala yanayowaadhiri. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Ili wateja sasa mjue mko na haki na wale wanaowahudumia wawahudumie sawa sawa kwa sababu ni haki yenu na mko kwa nchi huru ya jamhuri ya Kenya. Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** I want now to take you to Article 68, the rights of arrested persons; Article 68. Rights of arrested persons that is haki za watu wanao tiwa nguvuni. Inasema hivi; 68:1 “kila mtu anayetiwa nguvuni kwa madai ya kufanya kosa ana haki ya

(a) kubakia kimya” - Kuna hiyo haki

(b) kufahamishwa kikamilifu katika lugha anayoelewa”. Tuko pamoja? Hiyo lugha lazima iwe ni lugha ambayo unaelewa. Si kuambiwa unajua sheria Cap. hii inasema hivi, inasema hivi. Lazima umwambie wasi wasi inasema hivi kwa lugha ambayo unaelewa. Tuko pamoja? Tena inasema, “hata ingawa utabaki kimya” Pia sheria inasema, hapo (i) kuhusu haki ya kubaki kimya na kuhusu hadhari za kutobakia kimya. Pia utaambiwa hivyo.

Sasa hiyo ndiyo inaongea juu ya... (end of tape one)

Rights of persons held in custody; Page 10 article 70, tunataka kujua wale wako kwa custody kama hao pia wana haki. Haki za watu walio kisuisini; Article 71 inasema hivi “watu wote walio kizuizini chini ya sheria wawe wamehukumiwa au la wataendelea kuwa na haki zao chini ya Katiba isipokuwa haki hiyo iwe haiambatani na uhalisi wa kuwa kuwa kizuizini” Tuko pamoja?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Inginge mnaweza kusoma. I want now to take you to representation of the people; the electoral system and process. That is chapter 6 page 11 na nitasoma haraka sana Article 76: General principles of electoral system. Article 76 inasema hivi, as far as the draft Constitution is concerned: Uwakilishi wa watu; utaratibu wa upigaji kura: 76.1 “mfumo wa upigaji kura una msingi kuwa raia wote wana haki ya kupiga kura na kugombea uchaguzi wa Bunge na mashirika yenye mamlaka”. Tuko pamoja?

2. kupiga kura ni kwa siri

3. uchaguzi ni wa uhuru na haki

4. uchaguzi utahakikisha uwakilishi sawa wa watu

5. uchaguzi utahakikisha uwakilishi wa uhaki wa wanawake, walemavu na walio wachache.

6. uchaguzi utaendeshwa na shirika huru ambalo haliingiliwi kisiasa”. Tuko pamoja?

Then, I want to take you to Article 78.1, the right to vote; haki ya kupiga kura. Katiba mpya inasema hivi “raia mwenye umri wa miaka kumi na minane na zaidi ana haki ya kupiga kura.” Let us see page 12. Kwa hivyo hiyo ni haki ya kupiga kura.

Halafu tuangalie hapo chini Article 81 na inasema hivi “katika kila uchaguzi...” ninataka msikie kwa makini sana kwa sababu hapa ni muhimu hasa wakati huu ambao tunakaribia uchaguzi, na tuone hii swala Katiba mpya inasema nini kila saa inakaribia uchaguzi. “katika kila uchaguzi, tume ya uchaguzi itahakikisha kuwa

(a) utaratibu wa uchaguzi ni mwepesi na rahisi.” Tuko pamoja?

(b) Sanduku la kura ni angavu.” Right? Yaani the ballot box is transparent.

(c) Kura zinahesabiwa, zinaorodheshwa na kutangazwa na msimamizi kwenye kituo cha kupigia kura.” Right? Inatangazwa hapo hapo. Hakuna maana ya kupeleka pande zingine. Si hiyo ni kweli?

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Wacha tupige kura na hapoo mahali wanapigia kura, watangaze wazi wazi.

**Audience:** Ndiyo.

**Mr. Owade:** Kama ni elfu mbili ni elfu mbili.

**Audience:** Basi.

**Mr. Owade:** Si kupeleka mahali pengine. Haya! Tuone Article 82, the same page 12, tuone Katiba mpya inasema nini kuhusu wagombeaji bila kupingwa, yaani unopposed candidates. Tuone huu mswada unasema nini juu ya wagombeaji bila kupingwa. “mahali ambapo mgombeaji mmoja tu ndiye aliyependekezwa siku ya uteuzi kabla ya uchaguzi, hata hivyo uchaguzi utafanyika kwa minajili ya kuamua na kudhibitisha idadi ya kura ambacho kila chama cha kisiasa kimepata kwenye uchaguzi.

2. baada ya kura kuhesabiwa, mgombeaji atakuwa amechaguliwa” Sasa hiyo ndiyo inahusu Katiba mpya.

Halafu ninataka nisome tu kwa kifupi functions of the Electoral Commission, tujue hii Tume ya Uchaguzi, functions zake kwa Katiba mpya inasema nini. Article 84.1. “Tume ya uchaguzi ina wajibu wa;

- (a) Kusajili wa kuendelea wa wapiga kura” Sasa ile maneno ya ku-register voters tunataka iwe continuous, si ati iko tarehe fulani. Iwe tu kila wakati mtu anaweza ku-register. Tuko pamoja?
- (b) Kuweka mipaka ya maeneo ya Ubunge” Kwa sababu hii pia inaleta shida sana. Mpaka kwa eneo hili la Ubunge na lile. Si hiyo ni kweli?
- (c) Uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi na kura za maoni
- (d) Uendelezaji wa uchaguzi na kura za maoni, uhuru na zenye usawa
- (e) Usimamizi wa vyama wa kisiasa
- (f) Usimamizi wa mfuko wa fedha vya kisiasa
- (g) Usuluhishaji wa ubishi wa uchaguzi
- (h) Uendelezaji wa elimu ya uraia na utamaduni wa demokrasia
- (i) Kusaidia katika uchunguzi, ufuatili na utadhmini wa uchaguzi.

Hizo ndio zile authorities tumepatia Tume ya Uchaguzi kwa sababu tunataka hata vyama vya kisiasa viwe na discipline, vile

wanaendesha mambo yao. Si ati mtu anaamka tu anasema chama changu cha kisiasa ni hiki ama kile, chama ambacho hakina hata discipline. Tunataka Tume ya Uchaguzi iwe independent Commission ambayo inalinda na kuangalia sheria inasema nini kuhusu chama cha Kisiasa. Tuko Pamoja?

Tusome hapo kwa kifupi tu, the right to form a political party, Article 87.1 Haki ya kuunda chama cha kisiasa. Inasema “ kwa mujibu wa ibara 50, raia yeyote ana haki ya kuunda chama cha kisiasa

2. chama cha kisiasa kina haki ya msaada wa kifedha kutoka kwa serikali kwa msingi ulioagizwa na sheria ya Bunge.  
3. Hakuna mtu atakayetumia rasilmali za taifa kusaidia chama cha kisiasa.” Kwa hivyo ukisoma hizo zingine inahusu roles and functions of political parties, qualification for registration na tumeweka conditions ngumu sana na hizi conditions zikiwa fulfilled, tuna-predict kwamba with the coming into force of this Constitution, even after about twelve months, huenda tukawa na vyama tatu vya kisiasa pekee yake katika nchi hii ya Kenya na sasa mtasoma hapo kwa makini ili ujue inasema nini halafu maneno ya pesa na jinsi ya kutumia pesa ya chama cha kisiasa, unaweza kusoma hapo.

Pengine hata hapo kwa party discipline, Article 98. 1-4 inaongea kuhusu party discipline na ningependa tusome hapo. Nidhamu ya chama; “Katiba au ibara za ushirikiano za chama cha kisiasa itakuwa na masharti yatakayo hakikisha kuweko kwa nidhamu chamani na yanayo ambatana na kanuni za kidemokrasia, haki na uongozi wa kisheria.

2. chama cha kisiasa hakitamwadhibu mbunge wa chama kwa sababu ya jambo alilosema bungeni katika utumiaji wa fadhila za uhuru wa kutoa maoni bungeni  
3. chama cha kisiasa kitatekeleza shughuli zake kwa njia inayoendeleza demokrasia na siasa za amani. Tuko pamoja?

I want now to take you to chapter 7, Bunge; the Legislature. Am I too fast?

**Audience:** (Response not clear)

**Mr. Owade:** Okay. You will allow me at this juncture now to talk in English halafu nitajaribu kusema kwa Kizungu. Right? Kwa Kiswahili. This is a very sensitive area and because it is your right as a citizen, as a voter, it is important that you understand the new structure, which the Constitution of Kenya Review Commission is recommending on our Parliament. Are we together?

**Audience:** Yes.

**Mr. Owade:** I want to start by saying this, I will combine both devolution and Parliament and I would like to give you an overview of what it is all about. Having collected views of Kenyans in all the two hundred and ten Constituencies in this Country, having criss crossed various corners of this Country, wananchi had a lot of views on the structure of Parliament and we collected and collated those views and we came up as a Commission with the following recommendations. The

recommendation we made is that Parliament will be composed of two Houses; are we together? The first House will be known as the Upper House, the Upper House is the National Council, Bunge la Taifa. Ile ya pili tunaita the Lower House, in other words the National Assembly.

National Assembly is the one we have at the moment representing constituencies. They are 210 and the new Constitution is saying let the 210 remain as they are. Why? The national assembly represents two hundred and ten constituencies and the new Constitution is saying let us retain them as they are. The other House which is the Upper House is the National Council.

I now want to explain the structure and the composition. The National Council council shall be composed of a hundred Members of Parliament. Are we together? Out of these a hundred, 69 shall represent 69 districts in Kenya. In other words these districts, excluding Nairobi will send a representative to the National Council. Are we together? So, these 69 districts sending representatives to the National Council and Nairobi will send one, so the total will be 70. The other thirty, the Constitution of Kenya Review Commission is recommending, having listened to the views of Kenyans, let the seats be reserved for women. Are we together?

**Audience:** Yes.

**Mr. Owade:** Now how will this one be done? Kwa maswali tutauliza saa zingine tafadhali. How will this one be done? Thirty women will be elected directly according to provinces. Each province will elect four representatives. Are we together? So four representatives times seven comes to?

**Audience:** Twenty-eight.

**Mr. Owade:** Twenty-eight. The other two will come from Nairobi. So we are saying of the eight provinces, seven will present four representatives each but Nairobi will present two. In all these provinces, these women, the four representative, will be elected directly by people in that province. Are we together?

**Audience:** Yes.

**Mr. Owade:** So these representatives, the seventy, again we are saying they will be elected directly by the people in that district. So that is the composition of the National Council.

I want to go to another sensitive issue and I want you to listen very cautiously. In that Parliament, which is the current Parliament, which we now call the National assembly, we have added another group. This one is ninety and I want to explain what it is all about. Having listened to the views of Kenyans, majority of Kenyans according to our data felt that other sections

of the society need to be represented in that Parliament because they feel Parliamentarians when they go there they are just serving their own political interests apart from serving the interests of their constituents which some time they do not do so well, they just defend more of their political interests. Therefore, the youth in this Country said even us it is time we have a representative in Parliament, the disabled or persons with disability also felt they needed to be represented in Parliament, the marginalized groups, the ethnic groups or the small tribes, because in some regions you may go and you find that because you don't have enough population, the other dominant people or dominant ethnic groups or a dominant party will keep on winning all the time. Therefore the ethnic minorities or even some interest groups in our communities are not adequately represented. Ikiwa watu wa biashara, Chamber of Commerce and Industry for example, they also feel they need to articulate their interests in the National Assembly. So, we wanted now to balance, what do we do as a Commission? People said no, we need also to have proportional representation in Parliament. Having listened to all that, the Constitution of Kenya Review Commission recommended, let us ninety additional members in Parliament. How will this one be done? One year before every General Election, each registered political party in Kenya shall submit a list of 90 people to the Electoral Commission of Kenya. Are we together?

**Audience:** Yes.

**Mr. Owade:** Once they have submitted, even if they are a hundred political parties, they will submit but remember, there are very tough conditions which now the entrenched independent Electoral Commission will have to effect. Does that list have a national outlook? Does that list have somebody coming from North Eastern, Nyanza, Coast, Eastern, the whole Country? That is the first condition.

2. Does it have a priority? The disabled at the top? The youth, the marginalized groups or ethnic minorities? Special interest groups? That category must be fulfilled and it can be proved so that it is not a Luo, a Luyha, a Kikuyu or a Kalejiin, so that it does not belong to a particular class of people, the educated only or the uneducated only. So that it does not belong to all these people who are from a marginalized group. It must have a national image and national representative and the Electoral Commission will have to look into all that.

I now want to go to the question of whether they are nominated. I want to tell you here and now, in broad day light that you shall elect these people directly. How will you do this? During the voting day, and I want to dispel any misunderstanding to clarify issues which have been misunderstood because some people are opportunists and they fear that these people are going to rival them in Parliament, therefore they do not want them here. I want to clarify it this way: during the Election Day, the voting day, you shall vote twice in the ballot box.

Normally when you go to the constituencies, somebody might say you know me, I am just interested in a political party and not a candidate. Isn't it? Or, I am just interested in Honourable so and so and not the party. For example, may be if it is Ford Kenya, somebody says that my interest is just FORD – Kenya, and not a candidate or my interest is just in a candidate and not

FORD – Kenya. Isn't it? But we are now saying in the new Constitution, let us vote for the candidate and also let us vote for the party directly. Now, when we shall have the total overall votes in the whole Country, KANU for example, out of the total votes for the whole Country, KANU may have let us say in terms of the Party, leave alone the candidates now, in terms of parties, KANU may have let us say one million votes all over the Country, so let us say of the total votes of the whole Country, KANU gets 10% right? That 10% will be used against the ninety people so it means 10% of 90 is how many?

**Audience:** Nine.

**Mr. Owade:** So in this case, it means we give KANU nine seats. In other words, you have voted directly for the political party, so the number of votes the political party gets is what will be calculated against that number of ninety. In case KANU gets a hundred per cent of ninety, KANU will take all the ninety seats. Are we together?

**Audience:** Yes.

**Mr. Owade:** But then, there are conditions to be fulfilled, the youth have to be at the top, the disabled, the ethnic minorities, special interest groups, that is a condition which must be fulfilled to the Electoral Commission of Kenya, they will publish it in the newspaper, let it be open and everybody is aware of it. Are we together? In case there is no automatic winner, various political parties will get their seats in accordance with the percentage against the ninety seats. Are we together? It is difficult; I can see mama is looking at me. The coordinator will really have to explain to you so that you understand it. I want you to read it very carefully but that it is not complex as such. Parliament will have to work with the political parties that will come to enact laws which political parties will define these conditionality so that that list of ninety is maintained and one year prior to the general election, it has to be clear what groups have been classified here and then during the election day, you will vote. So, it means if you don't give respect for your political party, your political party will not get the ninety.

So, the more you vote for your political party, the more it gets seats in Parliament so it will be direct elections during the voting day. So you will vote twice on that particular day but that ninety must reflect a national outlook taking into account various interest groups in that priority in that order and you as a voter and a citizen of Kenya, you have a right to sue the political party or to sue the Electoral Commission, that is why we are saying one year prior to the election, the list must be out. Are we together?

**Audience:** Yes.

**Mr. Owade:** So, that is about it. I now want to take you to devolution. Devolution in Kiswahili, let me just refer; it is a bit difficult in Kiswahili. Devolution is in page 26 and I am combining devolution and Parliament together because they go hand in hand so that you understand what it is all about.

Devolution of power is in page 26 and I am not going to read all of this but I want just in brief to tell you that again as you are collecting views of Kenyans all over this Country, Kenyans felt that we need to bring the government closer to the people right from the village going to the top instead of coming to the top going down. Are we together?

**Audience:** Yes.

**Mr. Owade:** So the main reason is one, to bring the government closer to the people.

2. To make the people understand various structures of government because they will now be nearer to it, you are talking of a village government, a locational government, a district government. It is nearer to you as mwananchi of Kenya .

3. We want wananchi to have increased active participation in the management of their affairs. When you talk of separation of power, let that not be concentrated in a few hands, let us see power being distributed along various units to manage the people of Kenya and in order to provide efficient services to the people of Kenya. Are we together?

Therefore, I want us to read levels of government in page 26, Article 215. It reads as follows: “The powers are devolved to the following levels.

- (a) Village
- (b) Location
- (c) District and
- (d) Province.

Let us see what the village government is all about, 215.1: “the village decides whether the village Council is constituted by village elders through elections” Are we together? It is the village that decides whether the village council is constituted by village elders through elections.

- 2. The village council shall contain no less than six members and no more than ten members.
- 3. The village decides the system of village government including the role of the village Council.

Let us go to the Locational government, 217.1 “The Locational Council consists of two representatives, one of whom shall be a woman elected by each village council from among its members.

- 2. The location administrator is the Executive authority of the location.
- 3. The location administrator shall be elected by the registered voters of the location.

Let us go to the district government, 218.1 “ The legislative authority of the district is vested in the district council

2. The district Council consists of members directly elected by the registered voters of the district” This shall also be the Member of Parliament. You remember? “The district council shall consist of not less than 20 or more than 30 members.

3. The district administrator is the Executive authority of the district.

4. The district administrator is elected directly by the registered voters of the district
5. The district administrator with approval of the district council appoints chief officers from persons who are not members of the district council.
6. The district administrator can be dismissed by a vote of the majority of members of the district council that is supported in a referendum by a majority of those voting in the referendum.

Provincial government, 219.1: “The legislative authority of the province is vested in the provincial council.

2. The provincial council consists of two representatives one of whom shall be a woman chosen by each district council from among its members.

3. The provincial Executive committee consists of district administrators
4. The provincial administrator is the Executive authority of the province.
